# جبر الخواطروأثره على الفرد والمجتمع

# WEMA NA ATHARI ZAKE KWA MTU NA JAMII

## Imefasiriwa na

## Profesa.Ayman Alaasar

Shukra zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe wote, mwenye kusema ndani ya Kitabu chake Kitukufu {**Na tendeni mema ili mfanikiwe**} Na anasema {**Kauli njema na usamehevu ni bora kuliko sadaka inayo fuatiliwa na maudhi. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujitosha na Mpole**} Ninashuhudia kuwa hakuna Mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehema na amani kwa Mtume pamoja na Watu wake na Maswahaba zake na wale wenye kuwafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya utangulizi**:

Uislamu umekuja na ujumbe wenye kukusanya maadili yote bora na ya kupigiwa mfano, miongoni mwa maadili hayo bora ni pamoja na Wema na Ihisani, ambavyo ni ishara kubwa ya heshima ya nafsi, kwani Mwenyezi

Mungu Mtukufu amejiinua na sifa hii nzuri na akaifanya kuwa ni sifa katika sifa zake zinazohusiana na jina lake Tukufu nayo ni sifa ya "Mwenye kufanya atakalo" ambapo Anasema Mola Mtukufu: {**Yeye ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipokuwa Yeye tu. Mfalme, Mtakatifu, Mwenye salama, Mtoaji wa amani, Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake, Mwenye nguvu, Anaye fanya analo litaka**} huondoa umasikini kwa utajiri ugonjwa kwa afya hali ya wasi wasi na huzuni kwa matumaini, miongoni mwa maana ya jina hili kama alivyosema Imamu Al-Qurtwuby R.A ni mwenye kufanya kwa mwenye huzuni na kumpa utajiri masikini, na ilikuwa miongoni mwa maombi ya Mtume wetu Muhammad S.A.W ni pamoja na kusema "*Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe mimi na unirehemu uniongoze unifanyie niyatakayo na unipe riziki*".

Kama Mwenyezi Mungu alivyojitukuza kwa waja wake na kuwafanyia wema na kuzitia uzuri nafsi zao, huyu ni mama wa Nabii Musa A.S pale alipovunjika moyo juu ya mtoto wake kisha Mwenyezi Mungu alimrejeshea ambapo Anasema {**Basi tukamrudisha kwa mama yake ili macho yake yaburudike, wala asihuzunike. Na ajue ya**

**kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli, lakini wengi wao hawajui**}, na pindi Mtume S.A.W alipotolewa kwenye Mji wake wa Makka Mwenyezi Mungu alimfanyia wema na kumpa ufunuo akiwa njiani anaelekea Madina kwa kauli yake Mola Mtukufu {**Hakika aliye kulazimisha kuifuata Quran hapana shaka atakurudisha pahala pa marejeo**} kwa maana ya Mji wa Makka kwa mara nyengine.

Inaonekana wazi tabia ya wema katika maisha ya Mtume S.A.W pale aliporudi kwa mke wake Bi Khadija R.A akiwa anadhani kuwa amezungukwa na shari na mke wake akasema kumwambia ikiwa ni kuitia uzuri nafsi yake na nguvu ya wema kwake Mtume S.A.W akamwambia: Hapana, naapa Mwenyezi Mungu hatokudhalilisha kabisa, kwani wewe utakuwa ni mwenye kuunganisha undugu na kuyavumilia yote pamoja na kupata yasiyokuwepo, kuwafanyia upole wageni na kusaidia juu ya matukio ya haki, na pindi Mtume S.A.W alipokutana na Jabir Ibn Abdillah R.A akiwani mwenye huzuni kwa sababu ya kufariki shahidi baba yake mzee Abdillah R.A na kamwachia watoto na deni. Mtume S.A.W akamfanyia wema Jabir na kumwambia: *"Je nikubashirie yale*

*aliyokutana nayo baba yako?.....Mwenyezi Mungu hajazungumza na yeyote isipokuwa alizungumza naye nyuma ya kizuizi, amempa uhai baba yako na kuzungumza naye bila ya kizuizi na kumwambi: Ewe mja wangu unataka nini nikupatie, akasema: Ewe Mola, unirudishie uhai nikapigane kwa mara nyengine tena, ndipo Mwenyezi Mungu Mtukufu akamwambia kuwa imeshatangulia kauli kutoka kwangu kuwa hao kwenye huo uhai wa duniani hawatarejea tena*”.

Na Mtume S.A.W ametupigia mfano mkubwa katika wema na ihsani pale alipofikiwa na watu masikini waliohama Makka na wakamwambia: “*Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, watu matajiri wamekuwa wanafanya mambo yenye malipo, kwani wanaswali kama sisi tunavyoswali, wanafunga kama tunavyofunga, wanatoa sadaka katika mali zao zilizozidia, ndipo Mtume S.A.W akawaambia: Hivi Mwenyezi Mungu hakuwafanyia kitu cha kutoa sadaka? Kwani kila neno la kumtaja Mwenyezi Mungu ni sadaka, na kila neno la takbira ni sadaka, na kila neno la kumshukuru Mungu ni sadaka, kila neno la tahlil yaani kutamka* ***laa ilaaha illa llah*** *ni sadaka,*

*kuamrisha mema ni sadaka na kukataza maovu pia ni sadaka….*”.

Mwenye kuzingatia Sharia ya Kiislamu atakuta kuwa yenyewe imekuja na wema pamoja na ihisani kwa watu wote, hasa wale watu wanyonge ambapo Anasema Mola Mtukufu: {**Basi yatima usimwonee * Na anaye omba au kuuliza usimkaripie**} kwa maana ya wafanyie wema, na anasema Mtume wetu Muhammad S.A.W "*Hivi munadhani munapata ushindi na kuruzukiwa isipokuwa kwa sababu ya wanyonge wenu*" na anasema tena Mtume S.A.W "*Mimi na mlezi wa yatima Peponi tutakuwa kama hivi – akaashiria kidole cha shahada na cha kati*". Anasema tena Mtume S.A.W "*Mwenye kufanya juhudi kwa ajili ya wajane na masikini ni kama mtu mwenye kupigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, au mwenye kusimama usiku na kufunga mchana*". Na pindi Mtume alipoulizwa, ni matendo gani mema yaliyobora zaidi? Akasema: "*Ni kuleta furaha kwa ndugu yako Muislamu, au kumlipia deni, au kumlisha mkate*". Na akasema S.A.W "*Watu wenye kupendwa zaidi na Mwenyezi Mungu ni wale wenye kuwafaa watu, na matendo yenye kupendwa zaidi na Mwenyezi Mungu ni*

*kuleta furaha kwa Muislam, au kumuondolea tatizo lake, au kumlipia deni, au kumuondolea njaa, na nikiwa namtekelezea ndugu yangu hitajio lake ni jambo nilipendalo zaidi kuliko kukaa itikafu mwezi mzima ndani ya Msikiti huu wa Madina*".

**Khutuba ya Pili.**

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa ulimwengu, swala na salamu zimwendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume wetu Muhammad S.A.W pamoja na Watu wake na Maswahaba zake wote.

Hakuna shaka kuwa wema ni maadili yenye thamani kubwa yanayokusanya ulezi kwa jamii nzima, kwani Uislamu hautambui ubinafsi bali unatambua undugu wa kweli na kuchunga hisia za watu pamoja na kuwatendea wema, ambapo anasema Mtume wetu S.A.W: "*Mfano wa Waumini katika kupendana kwao kuhurumiana kwao na kufanyiwa kwao upole ni kama mfano wa mwili, kwani sehemu moja ya mwili inapohisi maumivu basi mwili mzima unahisi maumivu*". Na anasema Mtume S.A.W: "*Mwenye ziada ya alichobeba basi na ampunguzie yule asiye na kitu cha kubeba, na mwenye*

*ziada ya maandalizi basi na amwandalie yule aisiye na maandalizi yeyote*”.

Tunasisitiza kuwa wema kama unavyokuwa unaweza kuwa kwa neno jema, kwa dua ya kweli au kwa nasaha nzuri au kwa tabasamu jema, ambapo Mtume S.A.W anasema: “*Usidharau jema lolote hata kama ni kukutana na ndugu yako kwa sura ya tabasamu*”, kama tunavyosisitiza kuwa wema ni wenye athari kubwa katika kuunganisha nyoyo kuleta umoja na kuunganisha jamii.

**Ewe Mwenyezi Mungu turuzuku matendo mema na nguvu ya ihisan**.